**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**

**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MIUNDOMBINU**

**-----------------**

# TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MIUNDOMBINU KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026

*[Imetolewa kwa mujibu wa Kanuni 118 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023]*

**16 MEI, 2025**

# YALIYOMO

*Ukurasa*


**ORODHA YA VIELELEZO** ..... **ii**
**ORODHA YA VIFUPISHO NA MAANA** ..... iii
**SEHEMU YA KWANZA** ..... 1
**1.0 UTANGULIZI** ..... 1
1.1 Maelezo ya Awali ..... 1
1.2 Namna Kamati Iliyotekeleza Majukumu Yake ..... 2
**SEHEMU YA PILI** ..... 3
**2.0 UCHAMBUZI WA UTEKELEZAJI WA BAJETI PAMOJA NA MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025** ..... 3
2.1 Uchambuzi wa Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 ..... 3
2.2 Uchambuzi wa Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka 2024/2025 kuhusu Ukusanyaji wa Maduhuli ..... 5
2.3 Uchambuzi Kuhusu Upatikanaji wa Fedha hadi kufikia Mwezi Februari, 2025 ..... 6
2.4 Tathmini ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ..... 8
2.5 Ukaguzi wa Utekelezaji wa miradi ya Maendeleo iliyotengewa Fedha katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 ..... 9
2.5.1 Maelezo ya Awali ..... 9
2.5.2 Miradi iliyokaguliwa ..... 9
2.6 Maoni ya Jumla Kuhusu Utekelezaji wa Miradi iliyotembelewa na Kamati ..... 14
2.7 Uchambuzi wa Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara (Fungu 68) kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 ..... 16
2.8 Vipaumbele vya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 ..... 17
2.9 Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 ..... 17
2.10 Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 ..... 19
**SEHEMU YA TATU** ..... 21
**3.0 MAONI NA USHAURI** ..... 21
3.1 Maoni na Ushauri wa Jumla ..... 21
3.2 Maoni na Ushauri Mahususi ..... 22
**SEHEMU YA NNE** ..... 26
**4.0 HITIMISHO** ..... 26
4.1 Shukrani ..... 26
4.2 Msimamo wa Kamati Kuhusu Hoja ..... 28

## ORODHA YA VIELELEZO

**KIELELEZO NA 1:** Mchanganuo wa Hali ya Mapokezi ya Fedha za Miradi ya Maendeleo Kufikia Februari, 2025 ........ 6

**KIELELEZO NA 2:** Mchanganuo wa Hali ya Mapokezi ya Fedha za Miradi ya Maendeleo na Matumizi ya Kawaida kufikia Februari, 2025 ........ 7

**KIELELEZO NA 3:** Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026…………………… 18

**KIELELEZO NA 4:** Ulinganisho wa Bajeti ya Maendeleo na Matumizi ya Kawaida kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025- 2025/2026 ........ 19

## ORODHA YA VIFUPISHO NA MAANA

| | | |
|---|---|---|
| eGA | - | e - Government Authority |
| UCSAF | - | The Universal Communication Service Access Fund |
| TCRA | - | Tanzania Communication Regulatory Authority |
| TPC | - | Tanzania Postal Company |
| TTCL | - | Tanzania Telecommunication Company Limited |
| WHMTH | - | Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari |
| O.C | - | Other Charges |
| ICTC | - | ICT Commission |
| FTTH | - | Fibre to the Home |
| NIDC | - | National Internet Data Centre |
| TANESCO | - | Tanzania Electric Supply Company Limited |
| Wi-Fi | - | Wireless Fidelity |
| CCM | - | Chama cha Mapinduzi |
| DTP | - | Digital Tanzania Project |
| PDPC | - | Personal Data Protection Commission |

# SEHEMU YA KWANZA

## 1.0 UTANGULIZI

### 1.1 Maelezo ya Awali

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa **Kanuni ya 118 (9)** ya Kanuni za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu Kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**Mheshimiwa Spika**, taarifa hii imegawanyika katika sehemu kuu nne (4): -

(i) Sehemu ya Kwanza ni Utangulizi ambayo inaeleza kuhusu Muundo wa Taarifa pamoja na namna Kamati ilivyotekeleza majukumu yake;

(ii) Sehemu ya pili ni kuhusu uchambuzi na tathmini ya utekelezaji wa majukumu ya bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, pamoja na uchambuzi wa makadirio ya mapato na matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026;

(iii) Sehemu ya tatu ni maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati kwa Serikali; na

(iv) Sehemu ya nne ni hitimisho

## 1.2 Namna Kamati Iliyotekeleza Majukumu Yake

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu hutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia masharti mbalimbali yaliyoainishwa katika Katiba, Sheria mbalimbali pamoja na Kanuni za Kudumu za Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, katika kufanyia kazi utekelezaji wa Bajeti ya **Fungu 68 - Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Hanari** kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Kamati ilifanya yafuatayo: -

(a) Kupokea taarifa na kukagua utekelezaji wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 (Kanuni ya 117 (1));

(b) Kujadili utekelezaji wa Bajeti ya Wizara pamoja na taasisi zake kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 (Kanuni ya 117 (2);

(c) Kupokea na kufanya uchambuzi wa Randama ya Wizara (Kanuni ya 115 (1)); na

(d) Kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara pamoja na taasisi zake kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**SEHEMU YA PILI**

## 2.0 UCHAMBUZI WA UTEKELEZAJI WA BAJETI PAMOJA NA MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025

### 2.1 Uchambuzi wa Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025

**Mheshimiwa Spika,** wakati Bunge lako lilipopitisha bajeti ya **Fungu 68** kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Kamati ilitoa maoni na mapendekezo katika maeneo mbalimbali ili kuboresha utekelezaji wa bajeti ya Wizara hiyo.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kulitaarifu Bunge lako tukufu kwamba, Kamati imepitia taarifa ya utekelezaji wa maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati na kubaini kwamba, kuna baadhi ya maoni na ushauri wa Kamati ambayo utekelezaji wake ni endelevu na mengine hayajatekelezwa kikamilifu. Hivyo Kamati inasisitiza Serikali kufanyia kazi ushauri uliotolewa kama ifuatavyo: -

(a) Kamati ilishauri Serikali kuongeza kasi ya utekelezaji wa ujenzi wa vituo vya bunifu vya TEHAMA nchini. Napenda kulitaarifu Bunge lako tukufu kwamba, Serikali imeanza ujenzi wa vituo nane (8) vya kukuza bunifu za TEHAMA kwenye mikoa ya Dar es Salaam, Dodoma, Lindi, Mwanza, Arusha, Tanga, Mbeya, Mjini

Magharibi Zanzibar na kazi hiyo itakamilika mwezi Septemba, 2025.

(b) Kamati iliishauri Serikali kupitia upya mkataba wa ujenzi wa miundombinu ya njia ya Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano unaotekelezwa kati ya *TANESCO* na *TTCL.* Katika kutekeleza ushauri huu, Kamati imepokea taarifa kuwa, Shirika la Mawasiliano Tanzania *(TTCL)* na kampuni ya umeme ya *TANESCO* wamehuisha na kupanua wigo wa ushirikiano kupitia mkataba maalumu wa kibiashara ambao unatoa fursa sawa ya matumizi ya pamoja *(infrastructure sharing)* kwa taasisi zote mbili nchini kote. Aidha, mkataba husika umewasilishwa ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya upekuzi.

(c) Kamati iliishauri Serikali kuharakisha mchakato wa kupeleka Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano kwenye nchi jirani ikiwemo Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo ili kuongeza pato la Taifa. Kamati imetaarifiwa kwamba, mchakato wa suala hilo bado unaendelea. Kamati inaona kuwa kasi ya utekelezaji wa jambo hili ni ndogo hivyo msukumo unahitajika ili kukamilisha malengo ya mradi.

## 2.2 Uchambuzi wa Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka 2024/2025 kuhusu Ukusanyaji wa Maduhuli

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kwamba, Wizara hii iliidhinishiwa kukusanya **Sh. Bilioni 100.7** kutokana na Mauzo ya Huduma za Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano, na vyanzo vingine. Hadi kufikia Februari, 2025 Wizara ilikuwa imekusanya **Sh. Bilioni. 49.626** sawa na **asilimia 49.3** ya lengo.

**Mheshimiwa** Spika, kwa malengo ambayo Wizara ilijiwekea, ilitarajiwa kwamba, mauzo ya Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano pekee yangeweza kuipatia Wizara mapato ya takribani **Sh. Bilioni 80**. Hata hivyo, kiasi cha fedha kilichokusanywa kufikia Februari, 2025 ni **Sh. Bilioni 40.1** sawa na **asilimia 50** ya lengo.

**Mheshimiwa Spika,** kwa Upande wa taasisi zilizo chini ya Wizara, zilikadiriwa kukusanya **Sh. Bilioni 691.067**. Hadi kufikia Februari, 2025, Wizara ilikusanya **Sh. Bilioni 354.304** sawa na **asilimia 51.3** ya lengo.

**Mheshimiwa Spika**, kwa wastani hali ya makusanyo ya Wizara na taasisi zilizo chini yake sio ya kuridhisha kwani yapo chini ya wastani ambapo ni robo ya tatu ya Mwaka wa bajeti ilitakiwa angalau yafike wastani wa **asilimia 66.6**. Hata hivyo, kuna baadhi ya taasisi zilikusanya maduhuli kwa kiwango cha kuridhisha kama vile UCSAF **asilimia 92,** TCRA kwa **asilimia 79** na TCRA-CCC **asilimia 75**. Aidha, taasisi ambazo hazikuwa na makusanyo ya

kuridhisha hadi kufikia Februari, 2025 ni TTCL kwa **asilimia 35,** ICTC **asilimia 39**, Shirika la Posta **asilimia 44**, PDPC **asilimia 10.8**.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inazipongeza taasisi zilizofanya vizuri kwenye makusanyo na inaendelea kuishauri Serikali kuboresha mifumo ya makusanyo na ufuatiliaji ili kuongeza mapato ya Serikali, pia itathimini uwezo wa kila taasisi.

## 2.3 Uchambuzi Kuhusu Upatikanaji wa Fedha hadi kufikia Mwezi Februari, 2025

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari iliidhinishiwa jumla ya **Sh. Bilioni 180.926**. Kati ya Fedha hizo, **Sh. Bilioni 38.906** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Sh. Bilioni 142.019** kwa Miradi ya Maendeleo.

**KIELELEZO NA 1: MCHANGANUO WA HALI YA MAPOKEZI YA FEDHA ZA MIRADI YA MAENDELEO KUFIKIA FEBRUARI, 2025**

| BAJETI YA MAENDELEO | MAKADIRIO 2024/2025 | MAPOKEZI FEBRUARI, 2025 | % |
|---|---|---|---|
| FEDHA ZA NDANI | 116,469,894,000 | 64,013,787,953.93 | 54.96 |
| FEDHA ZA NJE | 25,550,000,000 | 31,837,415,900.00 | 124.60 |
| **JUMLA KUU** | **142,019,894,000** | **95,851,203,853.93** | **67.49** |

**Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia tarehe 28 Februari, 2025 Wizara ilikuwa imepokea jumla ya **Sh. Bilioni 118.515** sawa na **asilimia 65.5** ya lengo. Uchambuzi wa Kamati

umebaini kwamba, kati ya fedha zilizopokelewa, **Sh. Bilioni 22.663** ni fedha za matumizi ya kawaida sawa na **asilimia 58.25** ya bajeti iliyoidhinishwa na **Sh. Bilioni 95.851** zilipokelewa kwa ajili ya miradi ya maendeleo sawa na **asilimia 67.49** ya bajeti iliyoidhinishwa (**Kama inavyoonyesha kwenye Kielelezo Na.1)**

**KIELELEZO NA 2:** Mchanganuo wa Hali ya Mapokezi ya Fedha za Miradi ya Maendeleo na Matumizi ya Kawaida kufikia Februari, 2025

| BAJETI | MAKADIRIO 2024/2025 | MAPOKEZI FEBRUARI, 2025 | % |
|---|---|---|---|
| **1. MATUMIZI YA KAWAIDA** | | | |
| MISHAHARA | 24,997,474,000 | 12,708,698,377.33 | 50.8% |
| MATUMIZI MENGINEYO | 13,909,189,000 | 9,955,164,825.73 | 71.6% |
| **JUMLA (O.C)** | **38,906,663,000** | **22,663,863,203.06** | **58.25%** |
| **2. BAJETI YA MAENDELEO** | | | |
| FEDHA ZA NDANI | 116,469,894,000 | 64,013,787,953.93 | 54.96% |
| FEDHA ZA NJE | 25,550,000,000 | 31,837,415,900.00 | 124.60% |
| **JUMLA (MAENDELEO)** | **142,019,894,000** | **95,851,203,853.90** | **67.49%** |

**Mheshimiwa Spika**, kwa wastani, hali ya upatikanaji wa fedha kwa Wizara unaridhisha kwani hadi kufikia Februari, 2025, fedha iliyopokelewa ilikuwa ni wastani wa juu ya **asilimia 66.5.** Kamati inaendelea kuisisitiza Serikali kuhakikisha kwamba, fedha zote zilizoidhinishwa na Bunge zinatolewa kabla ya Mwaka wa fedha 2024/2025 kuisha.

## 2.4 Tathmini ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kwamba baadhi ya miradi ya maendeleo, ilipokea fedha kwa wakati na kuvuka matarajio wakati miradi mingine ilipokea fedha pungufu.

**Mheshimiwa Spika,** Mradi wa Tanzania ya Kidigitali ulipokea **asilimia 128** ya lengo hadi kufikia Februari, 2025. Fedha hizi ni kutoka nje zimewezesha ujenzi unaoendelea mfano ujenzi wa Minara ya Mawasiliano na utekelezaji wa Anwani za Makazi.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kwamba Mradi wa Mawasiliano Vijijini ulikuwa umepokea **asilimia 275.5** ya makadirio, na hivyo kuwezesha Serikali kusaini mkataba wa fedha mnamo tarehe 27 Septemba, 2024 baina ya Wizara ya Fedha na benki ya Exim ya China kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya mawasiliano nchini. Pia imewezesha ujenzi wa minara (*tower erection)* 108 kati ya 621 na minara 34 imeanza kutoa huduma.

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande mwingine, Kamati imebaini kwamba, miradi mingine ilikuwa imepokea fedha pungufu ambapo, kwa wastani, hadi kufikia Februari, 2025. Miradi hiyo ni Anwani za Makazi na Postikodi ulipokea **asilimia 10,** ujenzi wa Kituo Kikuu na Vituo Vidogo vya Kuendeleza Ubunifu katika TEHAMA *(ICT Park)* ulipokea **asilimia 18.7,** Kuimarisha Uwezo wa Taasisi katika utekelezaji wa majukumu ulipokea kwa

**asilimia 33.6,** Kuendeleza Ubunifu na Utengenezaji wa Vifaa vya TEHAMA ulipokea **asilimia 47.3** na ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano ulipokea **asilimia 50.**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwani wastani wa mapokezi ya fedha za miradi ya maendeleo ulikuwa ni wakuridhisha.

## 2.5 Ukaguzi wa Utekelezaji wa miradi ya Maendeleo iliyotengewa Fedha katika Mwaka wa Fedha 2024/2025

### 2.5.1 Maelezo ya Awali

**Mheshimiwa Spika**, katika kutathimini utekelezaji wa mpango wa maendeleo, kwa mujibu wa Kanuni ya 117 (1), Kamati ilifanya ziara ya ukaguzi ili kujionea utekelezaji wa miradi iliyopo chini ya Wizara hii iliyotengewa fedha katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 kama ifuatavyo:-

### 2.5.2 Miradi iliyokaguliwa

**(a) <u>Mradi wa maabara ya uidhinishaji wa vifaa vya Mawasiliano ya kielectroniki - TAL</u>**

**Mheshimiwa Spika**, dhumuni la uanzishwaji wa maabara hii ni kuhakikisha kuwa vifaa vya mawasiliano ya kielektroniki vinatengenezwa au kuingizwa nchini vinakidhi viwango vya kitaifa, kikanda na kimataifa.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipata fursa ya kutembelea mradi huo na kuelezwa kuwa, Tanzania ni moja kati ya nchi 12 barani Afrika ambazo zina maabara ya uidhinishaji wa vifaa vya mawasiliano ya kielektroniki, nchi hizo ni Tunisia, South Afrika, Ghana, Nigeria, Cameroon, Benin, Guinea, Togo, Senegal, Mali and Mauritania. Mradi huu ulianza kutekelezwa kuanzia mwezi Aprili, 2023 hadi tarehe 27 Machi, 2024.

**Mheshimiwa Spika**, gharama za mradi huu ni **Sh. Bilioni 7.527** mpaka sasa, kati ya fedha hizo **Sh. Bilioni 1.496** ni kwa ajili ya usanifu na ujenzi wa jengo la Maabara za Uidhinishaji wa Vifaa vya Mawasiliano, na **Sh. Bilioni 6.031** ni gharama ya ununuzi wa mitambo na usimikaji.

**Mheshimiwa Spika**, mpaka sasa mradi huu una maabara ya kupima mawimbi ya redio *(radio frequency)* na maabara ya kupima kiwango cha mionzi *(specific absorption rate)*.

**Mheshimiwa Spika**, tangu mwezi machi, 2024 tayari TCRA imefanikiwa kupima sampuli za vifaa 148 *(kwa modeli)* zikiwemo simu za mkononi na vishkwambi (*tablets)* na matokeo yalionyesha sampuli 6 hazikukidhi vigezo vya kutumika hapa nchi.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilibaini kuwa teknolojia inakua kwa kasi hivyo kupelekea mabadiliko ya mara kwa mara kwenye vifaa vya maabara ambavyo gharama yake ni kubwa.

**(b) <u>Mradi Na. 4292 - Ujenzi wa kituo kikuu na vituo vidogo vya kuendeleza ubunifu katika TEHAMA (ICT Park)</u>**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imeelezwa kuwa mradi huu ulitengewa kiasi cha **Sh. Bilioni 4,** hadi kufikia Februari 2025 fedha iliyopokelewa ni **Sh. Milioni 749.250** sawa na **asilimia 15.9** ya lengo.

**Mheshimiwa Spika**, mradi umepata mafanikio yafuatayo:-

(i) Kuandaa rasimu za miongozo mitano kwa ajili ya miundombinu muhimu ya TEHAMA, ambayo inajumuisha uendeshaji, usimamizi wa vihatarishi, ukaguzi, kukabiliana na majanga pamoja na mwongozo wa uhalisia na uadilifu wa data;

(ii) Kuandaa mkakakati wa taifa wa usalama mtandao ulioboreshwa; na

(iii) Kutoa elimu kwa umma kuhusu ulinzi na usalama wa mtandao katika mikoa ya

Dodoma, Morogoro, Dar es Salaam, Mwanza, Tabora na Zanzibar.

**Mheshimiwa Spika**, mradi una changamoto zifuatazo: -

(i) Kutokuwepo kwa sera na sheria inayohusu bunifu za TEHAMA; na

(ii) Fedha kuchelewa kutolewa kwa wakati hivyo, mkandarasi kutokamilisha ujenzi kwa wakati kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo malipo; na

**(c) <u>Kituo Cha Taifa cha Kutunza Data - (NIDC)</u>**

**Mheshimiwa Spika,** kituo hiki kinatoa huduma ya upangishaji wa nafasi *(Co-location/Virtual Server)*, uhifadhi (*storage)* na uwekaji wa tovuti mtandaoni (Web Hosting). Kituo kina mafanikio yafuatayo: -

(i) Hadi kufikia mwezi Februari, 2025 kituo kimeunganisha jumla ya wateja 211 ambao wanatumia huduma mbalimbali. Kati ya hao, wateja wa taasisi za Serikali ni 123 na taasisi binafsi ni 88;

(ii) Jumla ya mapato kwa kipindi cha Julai 2023 - Juni ,2024 yalikuwa ni kiasi cha **Sh. Bilioni 5.045.** Vile vile katika Mwaka wa Fedha 2024 /2025 matarajio yalikuwa ni kukusanya kiasi cha **Sh. Bilioni 7.253.** lakini hadi Disemba, 2024 kiasi

kilichokusanywa ni **Sh. 3.174.** sawa na **asilimia 43.7** ya lengo;

(iii) Kituo kinatarajia kuwa ifikapo tarehe 31 Juni, 2025 kitakuwa kimeunganisha wateja wapya 60 kati ya hao 30 watatoka taasisi na idara za Serikali na 30 kutoka kampuni binafsi;

(iv) Mkakati wa taifa wa uchumi wa kidigitali wa miaka (10) kuanzia 2024 - 2035 ulizinduliwa tarehe 29 Julai 2024 na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan (Rais) wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**Mheshimiwa Spika,** mradi unakabiliwa na changamoto zifuatazo: -

(i) Ukomo wa matumizi kwa baadhi ya vifaa vya miundombinu ya uendeshaji (life span);

(ii) Idadi ndogo ya vifaa vya kuhifadhia data (*racks)* ili kuendelea na utoaji wa huduma ya upangaji wa nafasi (colocation); na

(iii) Gharama kubwa za uendeshaji wa kituo cha kutunza data hasa matumizi makubwa ya umeme unaotumika kupooza vifaa na mitambo kutokana na jiografia yenye mazingira ya joto.

## 2.6 Maoni ya Jumla Kuhusu Utekelezaji wa Miradi iliyotembelewa na Kamati

### (a) Mtiririko wa Utoaji Fedha kwenye Baadhi ya Miradi

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kwamba, kuna changamoto ya utoaji wa fedha kwenye baadhi ya miradi kama vile mradi wa ujenzi wa jengo la Kituo Kikuu cha Ubunifu cha umoja wa kimataifa wa mawasiliano fedha zimepokelewa kwa **asilimia 18.7**, Anwani za Makazi na Postikodi kwa **asilimia 10**, Kuimarisha Uwezo wa Taasisi kwa **asilimia 33.6**, na Kuendeleza Ubunifu na Utengenezaji wa Vifaa vya TEHAMA kwa **asilimia 47.3.**

### (b) Ujenzi wa Minara ya Mawasiliano

**Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia Februari, 2025, UCSAF ilikuwa imekusanya kiasi cha **Sh. Bilioni 40.051** ambayo ni sawa na **asilimia 92** ya lengo. Makusanyo hayo ni kutoka vyanzo vya mapato, ambavyo ni ruzuku toka Serikalini, tozo za huduma, ruzuku toka TCRA na wadau wa maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kwamba, mfuko unaendelea na ujenzi wa minara 758 katika Kata 713 nchini. Hadi Februari, 2025 minara 443 imejengwa sawa na **asilimia 58.4.** Kati ya minara iliyojengwa, 417 sawa na **asilimia 55** inatoa huduma za

mawasiliano. Aidha, minara iliyobaki ipo katika hatua mbalimbali za ukamilishwaji.

**Mheshimiwa Spika,** wateja wa faiba (FTTH) 10,358 wameunganishwa sawa na **asilimia 8** ya lengo la nusu mwaka na **asilimia 4** ya lengo la mwaka.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa kuendelea kutenga fedha kwa ajili ya mradi huu na inaendelea kutoa ushauri kuwa fedha ziendelee kutolewa kwa wakati ili kukamilisha miradi.

**(c) Ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano kwenda Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC)**

**Mheshimiwa Spika,** moja kati ya jambo ambalo kamati ililifanyia tathimini ni ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano kutoka Tanzania hadi DRC. Kamati ilipokea taarifa kuwa, shirika limekamilisha uchambuzi wa zabuni na majadiliano ya mkataba kwa ajili ya ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano kuanzia Kigoma Tanzania hadi Kalemie, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC). Mkataba wa mradi husika umepelekwa kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya upekuzi na unatarajiwa kusainiwa Machi, 2025. Vile vile imepokea taarifa kuwa, utelekezaji wa mradi unatarajiwa kukamilika ifikapo Aprili, 2026.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na mafanikio yaliyofikiwa shirika linakabiliwa na changamoto ya uhaba na ubovu wa miundombinu ikiwemo barabara hususani maeneo ya vijijini.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaishauri Serikali kuharakisha ujenzi ili Mkongo ujengwe kwa manufaa ya kukuza uchumi wa nchi na kuongeza pato la Taifa**.**

## 2.7 Uchambuzi wa Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara (Fungu 68) kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 117 (2), Kamati ilifanya uchambuzi wake kwa kulinganisha makadirio ya matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 na Mwaka wa Fedha 2025/2026. Uchambuzi ulijielekeza katika maeneo yafuatayo: -

(a) Malengo ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026;

(b) Makadirio ya makusanyo ya maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026; na

(c) Makadirio ya matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

## 2.8 Vipaumbele vya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026

**Mheshimiwa Spika**, Wizara imeainisha vipaumbele mbalimbali kama ifuatavyo: -

(a) Kutunga, kuhuisha na kusimamia utekelezaji wa miongozo inayosimamia Sekta ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari;

(b) Kuimarisha upatikanaji wa huduma za mawasiliano ya simu na Posta kote nchini;

(c) Kuweka mazingira wezeshi kwa ajili ya kukuza na kuimarisha biashara Mtandao nchini;

(d) Kuimarisha miundombinu itakayowezesha utekelezaji wa Uchumi wa kidigitali;

(e) Kuimarisha ulinzi na usalama wa anga ya mtandao; na

(f) Kuweka mazingira wezeshi kwa ajili ya kuchochea ubunifu na kuimarisha ustawi wa kampuni changa *(startups)*.

## 2.9 Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026

**Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2025/2026,** Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari pamoja na taasisi zake inakadiria kukusanya **Sh. Bilioni 885.762** kiwango hiki ni ongezeko la **Sh. Bilioni 93.995** sawa na

**asilimia 11.87** ukilinganisha na **Sh. Bilioni 791.767** iliyopangwa kukusanywa katika Mwaka wa Fedha 2024/2025. **Kielelezo Na. 3** kinaonyesha mchanganuo wa makadirio ya makusanyo ya maduhuli hayo.

**KIELELEZO NA 3: Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026**

| NA | TAASISI | MAKADIRIO YA MAKUSANYO KWA MWAKA 2024/2025 (TZS) | MAKADIRIO YA MAKUSANYO KWA MWAKA 2025/2026 (TZS) | MAKUSANYO KUFIKIA FEBRRUARI, 2025 | ASILIMIA MAKUSANYO | TOFAUTI ya ASILIMIA (+/-) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | WIZARA | 100,700,000,000.00 | 100,369,242,950.00 | 49,626,389,613.00 | 49.3% | -0.33% |
| 2 | TCRA | 201,736,566,472.99 | 245,989,519,796.00 | 158,433,060,089.39 | 79% | +22% |
| 3 | TCRA – CCC | 710,000,000.00 | 710,000,000.00 | 532,500,000.00 | 75% | 0% |
| 4 | TTCL | 377,912,000,000.00 | 408,736,163,000.00 | 133,469,800,664.00 | 35% | +8% |
| 5 | TPC | 38,865,885,000.00 | 37,997,501,000 | 16,976,906,830.00 | 44% | -12% |
| 6 | UCSAF | 43,614,542,504.00 | 64,196,337,542.00 | 40,051,875,143.59 | 92% | +47% |
| 7 | ICTC | 6,428,707,300.00 | 6,718,050,253.92 | 2,486,439,962.00 | 39% | +4.5% |
| 8 | PDPC | 21,800,000,000.00 | 21,046,025,040.00 | 2,353,559,226.17 | 10.8% | -3.46% |
| | **JUMLA** | **791,767,701,276.99** | **885,762,839,581,92** | **403,930,531,528.15** | **51%** | **11.87%** |

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa kuongeza makadirio ya makusanyo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026. Kipekee, Kamati inazipongeza taasisi zilizopo chini ya Wizara, ambazo zimeongeza wigo wa makadirio ya makusanyo. Hatua hii itaongeza pato la Serikali na kuchochea uchumi.

## 2.10 Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, **Fungu 68** – Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Sh. Bilioni 291.533** ambapo kati ya fedha hizo, **Sh. Bilioni 14.485** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Sh. Bilioni 277. 047** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

**KIELELEZO NA 4: Ulinganisho wa Bajeti ya Maendeleo na Matumizi ya Kawaida kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025-2025/2026**

| MAELEZO | BAJETI YA MWAKA 2024/2025 | BAJETI YA MWAKA 2025/2026 | TOFAUTI (TZS) | TOFAUTI (%) |
|---|---|---|---|---|
| MATUMIZI YA KAWAIDA | 38,906,663,000 | 14,485,656,000 | -24,421,007,000 | -37% |
| MIRADI YA MAENDELEO | 142,019,894,000 | 277,047,483,000 | 135,027,589,000 | +195% |
| **JUMLA KUU** | **180,926,557,000** | **291,533,139,000** | **110,606,582,000** | **161.6%** |

**Mheshimiwa Spika,** bajeti ya Wizara imeongezeka kwa **Sh**. **Bilioni 110.606** sawa na **asilimia 161** kutoka **Sh. Bilioni 180.926** iliyotengwa katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 hadi kufikia **Sh. Bilioni 291.533** kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026. Fedha iliyotengwa kwa utekelezaji wa miradi ya maendeleo imeongezeka kwa **Sh. Bilioni 135.027** sawa na **asilimia 195** (kama ambavyo imeainishwa katika **Kielelezo Na. 4)**.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuongeza fedha za maendeleo na inatoa rai kwamba fedha zitolewe kwa wakati ili kuleta ufanisi katika utekelezaji wa vipaumbele vya Serikali kwa manufaa ya wananchi na Taifa kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa matumizi ya kawaida kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 bajeti imepungua kwa **Sh. Bilioni 24.421** sawa na **asilimia - 37**. ukilinganisha na bajeti hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 ambapo ilikuwa ni **Sh. Bilioni 38.906** ya sababu za punguzo hilo ni kutokana na mabadiliko yaliyofanyika ya Idara ya Habari na Maelezo kuhamishiwa Wizara ya Elimu na Mafunzo.

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, Wizara inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Sh. Bilioni 277.047** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ambayo ni nyongeza kwa **asilimia 195**. ukilinganisha na bajeti iliyotengwa kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025. Kati ya fedha hizo, **Sh. Bilioni 98.480** ni fedha za ndani, na **Sh. Bilioni 178.566** ni fedha za nje.

**SEHEMU YA TATU**

# 3.0 MAONI NA USHAURI

## 3.1 Maoni na Ushauri wa Jumla

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali kwa ufanisi mkubwa imeendelea kutoa Fedha za kutekeleza majukumu mbalimbali ya **Fungu 68** - Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, hususan katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kamati inaishauri Serikali: -

(a) Kuongeza ufanisi na ubunifu katika kuimarisha huduma za mawasiliano na kuhakikisha kuwa yanapatikana kwa urahisi kwa manufaa ya wananchi;

(b) Kuendelea kuweka mazingira wezeshi ya utendaji kazi utakaochochea kuboresha huduma za Sekta ya Mawasiliano na matumizi ya TEHAMA nchini, kwa kuwa sekta hiyo ni muhimu kwa maendeleo ya uchumi;

(c) Kuunganisha taasisi za Serikali na miundombinu ya mtandao wa kasi (*broadband infrastructure)*

(d) Kusimamia kikamilifu utekelezaji wa miradi yake yote ili iweze kuakisi viwango bora, uendelevu *(sustainability)* na kuwepo kwa thamani ya Fedha *(value for money)*; na

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inasisitiza usimamizi madhubuti kwa taasisi ili ziweze kujiendesha bila kutegemea ruzuku kutoka Serikalini na hatimaye kuboresha huduma za Mawasiliano na TEHAMA katika kuongeza mapato ya Serikali.

### 3.2 Maoni na Ushauri Mahususi

#### (a) Ulaghai katika Mitandao ya Mawasiliano

**Mheshimiwa Spika**, Katika "Ilani ya uchaguzi mkuu wa Mwaka 2020" Serikali, imeeleza nia ya kuimarisha mfumo wa TEHAMA wa udhibiti usalama na mapato katika Mawasiliano. Hata hivyo tatizo la uhalifu na utapeli kwenye mitandao ya mawasiliano bado linaendelea kwa kasi.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuwa, pamoja na hatua zinazoendelea kuchukuliwa na mamlaka husika, jitihada zaidi zinahitajika ili kutoa ufumbuzi wa kudumu sambamba na kuzuia jumbe fupi zinazotumwa bila idhini au matakwa ya mteja. Aidha, Wizara husika ishirikiane na makampuni ya mitandao ya simu pamoja na Wizara ya mambo ya ndani ili kumaliza tatizo hilo.

**(b) Fedha kutotolewa kwa wakati kwenye baadhi ya miradi iliyoko chini ya Wizara**

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na malengo mema ya kuanzishwa kwa mradi wa ujenzi wa vituo vya kuendeleza ubunifu na utengenezaji wa vifaa vya TEHAMA. Kuna changamoto kubwa ya upatikanaji wa Fedha kwenye miradi hii, hali hii inazoofisha jitihada za kukuza uchumi na kutatua tatizo la ajira kwa vijana nchini.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba fedha za miradi hiyo zinatolewa kwa wakati ili kufikia malengo kwa wakati.

**(c) Kutokuwepo kwa Sera na Sheria inayohusu bunifu za TEHAMA**

**Mheshimiwa Spika**, moja ya changamoto inayoikabili vituo vya bunifu za TEHAMA nchini ni kutokuwa na sera na Sheria katika suala la uendeshaji na usimamizi wa vituo hivyo, jambo linalopunguza kasi ya utekelezaji wa mradi huo.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaishauri Serikali kuleta bungeni Mswada utakaowezesha utungwaji wa Sheria husika ili kuweka mazingira wezeshi yenye kutoa ajira na kutambua bunifu za wananchi ipasavyo. Aidha, ujenzi wa vituo hivyo uende sambamba na kuongeza

idadi ya Wataalam na Wakufunzi wa kuendesha vituo hivyo ili iweze kuleta tija iliyokusudiwa.

**(d) Gharama Kubwa za Uendeshaji wa Kituo cha Kutunza Data.**

**Mheshimiwa Spika**, kumekuwa na changamoto katika uendeshaji wa mradi wa vituo vya kutunzia data nchini, kunakosababishwa na matumizi makubwa ya umeme, ukomo wa matumizi wa baadhi ya vifaa vya miundombinu ya uendeshaji wa kituo cha kutunzia data *(life span)* na idadi ndogo ya vifaa vya kuhifadhia data *(racks)* ili kuendelea na utoaji wa huduma ya upangaji wa nafasi *(colocation)*. Hali hii inasababisha uwepo wa gharama kubwa katika uendeshaji.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaishauri Serikali kufanya utafiti wa kutosha ili kubaini eneo lenye mazingira rafiki yenye hali ya baridi ili kujenga kituo kipya, hii itasaidia kupunguza gharama za umeme unaotumika kuendesha mitambo.

**(e) Kutumia Fursa ya kuwa na maabara ya vifaa vya mawasiliano ya kieletroniki**

**Mheshimiwa Spika,** imebainika kuwa, Tanzania ndiyo nchi pekee inayomiliki mtambo wa upimaji wa bidhaa za kielectroniki katika ukanda wa nchi za Afrika

Mashariki, fursa hii ikitumiwa vizuri inaweza ikaingiza kiasi cha fedha kutoka kwa majirani zetu ambao hawana aina hii ya maabara, hivyo basi, Kamati inaishauri Serikali kutumia fursa hii ipasavyo ili kuongeza pato la nchi,

**Mheshimiwa Spika,** Serikali iziunganishe mamlaka za udhibiti ubora wa bidhaa nchini kwa kutumia mfumo wa pamoja *(one single system*) ili kuleta uthibiti wa bidhaa za kielektoniki nchini, pia ifanye ukaguzi wa mara kwa mara kwa watumiaji wa vifaa hivyo na kubaini kama kuna ukiukwaji wowote ili kuondoa athari zinazoweza kutokea katika jamii.

## SEHEMU YA NNE

# 4.0 HITIMISHO

## 4.1 Shukrani

**Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya kipekee naendelea kukushukuru wewe binafsi kwa kuendelea kuliongoza vyema Bunge letu na kwa maelekezo yako ambayo yamekuwa msaada mkubwa katika uendeshaji bora wa shughuli za kila siku za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu. Aidha, namshukuru Naibu Spika, kwa namna anavyokusaidia kutekeleza majukumu yako, pamoja na wenyeviti wa Bunge kwa kukusaidia kuendesha kwa ufanisi vikao vya Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, kwa moyo wa dhati kabisa, niwashukuru sana wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu ambao wamekuwa mstari wa mbele katika kuendelea kuisimamia Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari pamoja na taasisi zilizo chini yake kwa niaba ya Bunge lako tukufu. Kwa hakika, maoni, ushauri na mapendekezo yao vina mchango mkubwa katika kuboresha utendaji wa Serikali. Naomba niwatambue wajumbe hao ili majina yao yaingie katika Kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge *(Hansard)* kama ifuatavyo: -

1. Mhe. Moshi Selemani Kakoso, Mb. - **Mwenyekiti**
2. Mhe. Anne Kilango Malecela, Mb. - **Makamu**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 3. | Mhe. Kapt. Abbas Ali Hassan Mwinyi, Mb. | - | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Abdallah Jafari Chaurembo, Mb. | - | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Abubakar Damian Asenga, Mb. | - | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Ahmed Mabkhut Shabiby, Mb. | - | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Ally Anyigulile Mlaghila Jumbe, Mb. | - | Mjumbe |
| 8. | Mhe. Amina Ali Mzee, Mb. | - | Mjumbe |
| 9. | Mhe. Angelina Adam Malembeka, Mb. | - | Mjumbe |
| 10. | Mhe. Fredrick Edward Lowassa, Mb. | - | Mjumbe |
| 11. | Mhe. Geoffrey Idelphonce Mwambe, Mb. | - | Mjumbe |
| 12. | Mhe. Ghati Zephania Chomete, Mb. | - | Mjumbe |
| 13. | Mhe. Innocent Edward Kalogeris, Mb. | - | Mjumbe |
| 14. | Mhe. Prof. Joyce Lazaro Ndalichako Mb. | - | Mjumbe |
| 15. | Mhe. Livingstone Joseph Lusinde, Mb. | - | Mjumbe |
| 16. | Mhe. Mbarouk Juma Khatib, Mb. | - | Mjumbe |
| 17. | Mhe. Miraji Jumanne Mtaturu, Mb. | - | Mjumbe |
| 18. | Mhe. Mohamed Maulid Ali, Mb. | - | Mjumbe |
| 19. | Mhe. Eng. Mwanaisha Ng'anzi Ulenge, Mb | - | Mjumbe |
| 20. | Mhe. Mwatumu Dau Haji, Mb. | - | Mjumbe |
| 21. | Mhe. Stella Simon Fiyao, Mb. | - | Mjumbe |
| 22. | Mhe. Sylvia Francis Sigula, Mb. | - | Mjumbe |

**Mheshimiwa Spika**, naomba nitumie fursa hii kumshukuru sana Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mhe. Jerry W. Silaa, (Mb) kwa ushirikiano ambao ameipatia Kamati katika kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu ya Kamati akisaidiwa na Naibu Waziri wake, Mhe. Mhandisi Maryprisca Mahundi (Mb).

Aidha, niwashukuru watendaji wote wa Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari pamoja na taasisi zake chini ya uongozi wa Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Bw. Mohammed Khamis Abdullah, Kamati inatambua mchango wa watendaji hao katika maendeleo ya Sekta ya Mawasiliano na TEHAMA na inaendelea kuwatia moyo kwamba wafanye kazi kwa bidii.

**Mheshimiwa Spika**, mwisho lakini sio kwa umuhimu, nawashukuru sana watendaji wote wa ofisi ya Bunge chini ya uongozi wa Katibu wa Bunge, Bw. Baraka I. Leonard kwa kuisaidia Kamati kutekeleza majukumu yake hadi kukamilika kwa Taarifa hii.

## 4.2 Msimamo wa Kamati Kuhusu Hoja

**Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo, naomba Bunge lako likubali kupokea na kupitisha makadirio ya mapato na matumizi ya **Fungu 68 – Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari** kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

Moshi Selemani Kakoso, Mb.

**MWENYEKITI**

Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu

16 Mei, 2025